TANGAZO LA SERIKALI NA. 336 la Tarehe 20/07/2018

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

SURA 290

# SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 6(1) na 16(1)*

SHERIA NDOGO (USHURU WA MAEGESHO) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI ZA MWAKA, 2018

Jina na mwanzo wa kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo (Ushuru wa Maegesho) za Halmashauri ya Manispaa kigamboni za 2018 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa Kigamboni.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:-

*"Afisa Mwidhiniwa"* maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

*"Halmashauri"* maana yake Halmashauri ya Manispaa Kigamboni;

*"Mkurugenzi"* maana yake ni Mkurugenzi wa Manispaa Kigamboni pamoja na afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

*"Maegesho"* maana yake ni eneo maalum lililotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kutolea huduma za usafiri ambapo mabasi au vyombo vingine vya usafirishaji wa abiria vitapakia au kushusha abiria na mizigo yao;

*"Maegesho maalum"* maana yake ni sehemu maalum iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha magari kwa utaratibu maalum uliowekwa katika kifungu cha (8)

cha Sheria Ndogo hizi;

*"Yadi"* maana yake ni eneo la Halmashauri lililotengwa kwa ajili ya shughuli za ufundi na kuhifadhi vyombo vya usafiri.

Ushuru wa maegesho

4. (1)Halmashauri itatenga na kuanzisha maeneo ya maegesho kwa vyombo vya usafiri vitakavyoegeshwa katika maeneo yalio ainishwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Halmashauri itatoza ushuru wa maegesho kwa mujibu wa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

Namna ya kutoza ushuru wa maegesho

5. (1) Ushuru wa maegesho utatozwa kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni kila siku.

(2) Ushuru wa maegesho utalipwa kwa kila siku au mwezi kadri Halmashauri itakavyoona inafaa.

(3) Halmashauri inaweza kukubaliana kuwa na utaratibu maalum wa namna ya kulipa ushuru wa maegesho na wadau wake.

(4) Ushuru wa maegesho utalipwa na mtu yeyote mara tu anapoegesha chombo cha usafiri.

(5) Endapo mtu yeyote amelipa ushuru wa maegesho kwa siku au kwa mwezi ataruhusiwa kuegesha chombo cha usafiri alicholipia katika eneo lolote lililoainishwa kwa ajili ya maegesho ndani ya halmashauri kwa muda aliolipia.

Msamaha wa Ushuru

6. Bila kuathiri masharti ya kifungu cha 5(4) hapo vyombo vya usafiri vya Serikali, wanadiplomasia, Majeshi, na magari ya kubeba wagonjwa havitatozwa ushuru wa maegesho.

Mamlaka ya Halmashauri

7. (1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kukamata na kuondoa chombo cha usafiri kilichoegeshwa kwenye eneo ambalo halikuainishwa katika Sheria Ndogo hizi.

(2) Chombo cha usafiri kilichokamatwa kwa mujibu wa kifungu cha 7(1) kitaondolewa na kuhifadhiwa katika yadi ya Halmashauri au sehemu yeyote iliyoainishwa na Halmashauri na kutozwa kiasi cha shilingi elfu hamsini kwa siku.

(3) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuuza chombo cha usafiri endapo mmiliki wa chombo hicho atashindwa kulipa

gharama za kuondoa chombo cha usafiri ndani ya kipindi cha siku 14 tangu tarehe ya kukamatwa baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(4) Halmashauri baada ya kupata idhini ya Mahakama itakiuza chombo husika kwa kuzingatia bei ya soko na kiasi kitakachopatikana kitakatwa deni linalodaiwa na Halmashauri na kiasi kinachobaki atakabidhiwa mmiliki wa chombo.

Maegesho maalum

8. Halmashauri inaweza kutenga eneo maalum la maegesho ya vyombo vya usafiri na kutoza Ushuru wa Maegesho kwa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.

Makosa

9. Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote endapo:-

(1) atashindwa kulipa ushuru wa maegesho.

(2) atamshawishi mtu yeyote au kundi la watu kutolipa Ushuru wa maegesho.

(3) ataegesha chombo cha usafiri katika eneo ambalo halijaainishwa na halmashauri.

(4) ataosha au kufanya matengenezo ya chombo cha usafiri katika eneo la maegesho.

Kufifilisha kosa

10. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza faini mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria hizi, kiasi kisicho pungua (Tsh.200, 000/=) na kisichozidi shilingi laki tano (Tsh. 500,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoambatishwa kwenye jedwali la tatu la Sheria Ndogo hizi, na atatakiwa kulipa ushuru anaodaiwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Adhabu

11. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua (T.sh. 200,000/=) na isiyozidi shilingi milioni moja (Tsh. 1,000,000/=) au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote kwa pamoja na faini na kifungo.

JEDWALI LA KWANZA

*Limetungwa chini ya kifungu cha 4(2)*

USHURU WA MAEGESHO

| *AINA YA GARI* | *USHURU* |
|---|---|
| | *Kwa siku* |
| Gari ya Mizigo zaidi ya Tani 5 | 3,000/= |
| Gari la Mizigo chini ya Tani 5 | 2,000/= |
| Gari Ndogo/ taxi | 1500/= |
| Pick up/Station Wagon | 2,000/= |
| Daladala kwa kila safar moja | 5 00/= |

JEDWALI LA PILI

*Limetungwa chini ya Kifungu cha 8*

MAENEO YA MAEGESHO MAALUM

| *Na* | *AINA YA CHOMBO CHA USAFIRI* | *USHURU* |
|---|---|---|
| 1. | MAGARI MAKUBWA ZAIDI YA TANI 3 NA NUSU | 5,000/= |
| 2. | MAGARI MADOGO CHINI YA TANI TATU | 2,500/= |
| 3. | MABASI MAKUBWA YENYE ABIRIA 65 NA KUENDELEA | 5,000/= |
| 4. | MABASI MADOGO YA MZUNGUKO WA KILA SIKU | 1,500/= |
| 5. | MABASI MADOGO YENYE UWEZO WA KUCHUKUWA ABIRIA 1-40 | 2,500/= |
| 6. | MAGARI MAKUIBWA YA MIZIGO YENYE TAN 1O NA KUENDELEA | 10,000/= |
| 7. | TOZO YA ADA MAALUM KWA MWAKA | 300,000/= |

JEDWALI LA TATU

HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

*(Chini ya kifungu cha 10)*

Mimi ........................ nakiri mbele ya ............ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashuri ya Manispaa Kigamboni kwamba mnamo tarehe ...... ya Mwezi ....... Mwaka ...... nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha ...... cha Sheria Ndogo za (Ushuru wa Maegesho ) za Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni za Mwaka 2018.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa Kigamboni, niko tayari kulipa kiasi cha ushuru ninaodaiwa pamoja na faini iliyoelekezwa kwenye Kifungu 10 cha Sheria Ndogo hizi.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe............ ya Mwezi........... Mwaka .....................

*Jina*.................................... *Saini*..........................................

Mbele ya :

Jina: ..................................................

Cheo: ...............................................

Saini: ...............................................

Nembo ya Halmashauri ya Manispaa Kigamboni imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika mnamo tarehe 31 Januari, 2018 mbele ya:-

STEPHEN E. KATEMBA
*Mkurugenzi,*
*Halmashauri ya Manispaa Kigamboni.*

L.S

MAABAD SULEIMAN HOJA
*Mstahiki Meya*
*Halmashauri ya Manispaa Kigamboni.*

NAKUBALI

Dodoma,
07 Juni, 2018

MHE. SELEMANI S. JAFO (MB.)
*Waziri wa Nchi/OR -TAMISEMI.*